MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA
WAKRISTADELPHIANO NA 20.

ROHO MTAKATIFU WA MUNGU

Soma: Marko 1

> *"Mungu akasema, na iwe nuru: na ikawa nuru" (Mwanzo 1:3)*

Inaonekana kuwa ni rahisi mno. Lakina fikiria nguvu kubwa na maarifa yalio hitajika kabla ya nuru kuweza kuumbwa.

> *"Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi" (Mwanzo 1:1)*

Fikiri tena, kazi zote ambazo inabidi zifanyike ili kujenga nyumba. Fikiria mipango yote na matayisho; mahitaji ya watu walio na ujuzi katika shughuli tofauti, wote wakifanya kazi pamoja. Ushauri gani mw mwingi na itachukua!
Mawazo na nguvu kiasi gani, wakati ule, ilibidi ichukue kuumba mbingu na nchi? wa kazi hii kubwa uwezo ulitoka wapi?
Tuna ambiwa katika Zaburi:

> *"Kwa neno la Bwana mbingu zilifanyika; na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake.....kwa maana alisema, ikafanyika; aliamuru, nayo ikasimama" (Zaburi 33:6,9)*

Mwanzo 1:2 inatuonyesha kwamba **Roho ya Mungu ilitumika kwenye uumbaji:**

> *"Roho ya Mungu ilisogea juu ya uso wa maji".*

Maongozi na Roho ya Mungu
Uwezo wa Mungu pia ulitumika kuongoza fikra za watu walio andika Biblia. Hii ime julikana kama 'maongozi'. Mungu aliwatumia watu kuandika Neno Lake.

(b) Utakuwa lili;
(c) Utapatikana vipi.

23C Yapi kati ya haya yanamaanisha ‘kaburi’?
(a) Hades;
(b) Jehanamu;
(c) Sheol;
(d) Roho;
(e) Kuzimu.

23D Kazi ya ziada
Chahua maneno toka kwenye orodha mwishoni ili ujaze nafasi katika fungu la maneno chini ambalo lipo katika Zaburi 16:10 na Matendo 2:27 _____ hakuiacha _____ ya _____ katika _____, wala, wala Yeye _____ hakuruhusu _____ wa Yesu _____.

Orodha ya kuchagua (Utahitajika katumia baadhi zaidi ya mara moja): mwili, roho, Yesu, kaburi, kuoza, teseka, Mungu, kuzimu, Daudi.
Kitu gani kilikuwa kinatajwa katika tukio la maisha ya Yesu.

Tuma majibu yako kwa:

Jina lako ni:

Hivyo tunasoma katika 2 Petro 1:21:

> *"Unabii haukuja wakati wa zamani kwa mapenzi ya mwanadamu; bali watakatifu wa Mungu walisema kama walivyo ongozwa na Roho Mtakatifu".*

Unabii siku yote haumaanishi kuena ya wakati ujao. Katika biblia una maana ya kusema maneno ya Mungu, kama kuhusu wakati uliopita, uliopo au ujao.

Waandishi 30 waliandika maneno ya Biblia zaidi ya miaka karibu 1500. Kama Mungu hakuwaongoza kuandika Biblia wakati huo ingekuwa ni mchanganyiko wa mawazo na kawaida.
Badala yake Biblia ina maneno makuu mwendo wote moja kwa moja hata mwisho. Yenyewe haipingani au kutofautiana.

Hapa kuna baadhi ya vitu tumeambiwa kuhusu Roho ya Mungu:

1.	Roho ya Mungu inaweza kuumba	Kama katika Mwanzo 1:2
2.	Mungu, kwa Roho yake ajua vyote	Zaburi 139:2-12
3.	Kwa Roho Yake viumbe vipo hai	Zaburi 104:29-30 na Ayubu 26:13
4.	Roho ya Mungu iliwasaidia watu kufanya mapenzi yake	Waamuzi 6:34; 11:29; Wagalatia 5:16
5.	Manabii walijua cha kusema kwa kupitia Roho ya Mungu	Mika 3:8; Zakaria 7:12; Nehemia 9:30: 2 Petro 1:21

Nini maana ya maneno "Roho Mtaktifu"?

Fungu la maneno 'Roho Mtakatifu' linapatikana kweye Biblia.

Mtakatifu maana yake *"weka mbali"* au *"iliyo peke yake",* na "kutenga" kwa madhumuni maalum.

Kwa hivi tunataja uwezo mkuu wa Mungu kama "Roho Mtakatifu", na kama Mtume Petro alivyo sema katika 2 Petro 1:21:

> *"Unabii huakuja wakati wa zamani kwa mapenzi ya mwanadamu, bali watakatifu wa Mungu walinena kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu".*

Katika biblia Roho wa Mungu au Roho Mtakatifu, ni nguvu za Mungu; ni uwenzo I ambao Mungu anao utumia kutimiza mapenzi Yake na mipango.

Roho Mtakatifu na Yesu Kristo Bwana

Ilikuwa ni Roho Mtakatifu aliye leta kuzaliwa Bwana Yesu. Kwa hivyo Mariamu aliambiwa na malaika:

> *"Sasa kuzaliwa kwa Yesu Kristo ilikuwa hivi; Wakati mama yake alipokuwa ameposwa kwa Yusufu, kabla hawajakuwa pamoja, alikutwa ana mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu"*
>
> *(Mathayo 1:18).*

Kwenye ubatizo wake katika Mto Yordani, Yesu alipewa Roho Mtakatifu bila kipimo (yaani, pasipo mpaka wowote ule). Tunasoma kwa Yohana 3:34 :

> *"Ambaye Mungu amemtuma ananena maneno ya Mungu: kwa maana Mungu hampi Roho kwa kipimo."*

Uwezo wote alipewa Yesu. Kwa watu wengine wa nyakati za Agano la Kale na Jipya, Mungu aliwapa sehemu ya uwezo Wake - lakini hajawahi kuwepo mtu mwingine anaye faa kushika uwezo kama huu kama Mungu alio mpa Yesu. Yesu aliweza kuutumia uwezo huu mkuu kwa kutenda miujiza na ulisaidia mahubiri yake.

Tazama maneno haya kutoka Isaya 61:1,2:

MASWALI KARATASI YA 6

Jaribu na ujibu maswali kwa maneno yako mwenyewe. Kwenye ‘kazi ya ziada’ unaweza kujibu swali kama unataka, au kuacha ikiwa utaona ni ngumu sana. Tafadhali jaribu kujibu maswali mengine yote.

MASOMO 20-23

20A Nakili na ukamilishe fungu hili la maneno. (Utahitaji zaidi ya neno 1 kwenye nafsi zingine): _____ Mtakatifu ni _____ wa Mungu. Mungu _____ mbingu na nchi kwa kutumia Roho wake. Maneno ya Biblia alitaka yaandikwe. Alimtumia _____ wake kuwaambia watu yapasayo kuandikwa. Hii imeitwa ni _____. _____ alipata mimba ya kumzaa Yesu kwa tendo la Roho Mtakatifu, na kisha Yesu alipewa Roho Mtakatifu wakati _____. Alitumia uwezo huu _____.’Mfariji’ ni _____ na aliwasaidia _____ kwa kuwakumbusha yale Yesu aliyo waambia. Tunasoma hili kwa kupewa kwao katika Matendo sura _____. Ilitolewa baada ya Yesu _____.

21A Zawadi za Roho Mtakatifu zilikuwa kwa ajili ya nini?
21B Zilidumu kwa muda gani?
21C Zawadi zipi zilikuwa ni za muhimu zaidi?
21D Zawadi gani ni za muhiumu zaidi kuliko zote? (1 Wakorintho 13)
21E Watu gani walikuwa na uwezo wa kutoa zawadi hizi za Roho Mtakatifu?
21F Zawadi za Roho Mtakatifu zipo leo?

22A Biblia inatuambiaje kuhusu Adamu alivyo umbwa?
22B Eva aliumbwa vipi?
22C Je, nyoka alimfanya Adamu na Eva kula matunda yaliokatazwa?
22D Adamu alipata adhabu gani kwa kumwasi Mungu?
22E Kwa nini watu wote wanakufa?
23A Panatokea nini mtu afapo?
23B Kuna uzima baada ya mauti? Kama ndivyo, sema
(a) Utakuwa wapi;

“Hades” kama tulivyo kwisha ona ni neno la Kiyunani maana yake ni kaburi.

Jehanamu inahusu nini?
Yesu anasema mara tatu katika Marko 9 “moto usio zimika”. Anasema:

> *“Ni afadhali kuingia katika uzima u kigutu, kuliko kuwa na mikono miwili na kwenda jehanamu, kwenye moto usio zimika” (mstari 43).*

Bado tunajuwa kwamba wafu huwa hawana fahamu na hawajui lolote. Yesu alikuwa ana maana gani?
Jehanamu ni neno linalo toka katika Kiebrania **Ghi-Hinnom.** Hili lilikuwa ni jina la bonde nje ye mji wa Yerusalemu ambako zamani kabla Wafalme wa Israeli hasa walipo choma watoto wao kama sadaka kwa miungu migeni. (Unaweza kusoma kwa 2 Wafalme 23:10).

Katika wakati wa Yesu, bonde hili la Hinnom lilikuwa ni mahali ambapo mizoga ya wanyama na takataka za mji vilichomwa. Moto uliwaka daima. Palikuwa ni mahali pa kuteketeza kabisa. Hivyo wakati Yesu anatumia neno Jehanamu, watu walilifikiria bonde hili na kutambua kwamba alitumia mfano kamili na kuharibu kabisa.
Alikuwa **hasemi** watu watateswa milele.

Muhutasari

Biblia inafundisha kwamba mauti ni mwisho wa ufahamu wa uzima wote.
Haitoi ahadi ya kwenda mbinguni.
Ina ahidi kwamba Yesu atarudi na kufufua wafu.
Wakati huo, atawapa uzima wa milele wafuasi wake waaminifu.
“Kuzimu” ni kaburi; mahala wanapo zikwa wafu.
Jehanamu ni bonde lililo karibu na Yerusalemu mahali taka zichomwapo: katika Biblia lina maana kuteketeza kabisa.

Sura ya kusoma: Yohana 11:1-45
Mstari wa kujifunza: 1 Wakorintho 15:22-23

> *“Maana kama katika Adamu wote hufa, kadhalika wote katika Kristo watafanywa wawe hai: Kristo ni wa kwanza; baadaye walio wake Kristo atakapokuja.”*

> *"Roho wa Bwana Mungu yu juu yangu, kwasababu BWANA amenipaka mafuta kuhubiri .....kuwafunga walio vunjika moyo..... kuwatangazia uhuru mateka ..... kuwafariji wanao lia".*

Soma sura nzima kutoka kwenye Biblia yako. Hii ni picha ya Yesu akitumia Roho wa Mungu katika kazi yake. Hakumtumia Roho kwa kujihudumia mwenyewe, bali kuwasaidia wengine.

Wanafunzi waliahidiwa Roho Mtakatifu

Yesu aliwaahidi wanafunzi wake kumi na mbili kwamba pia nao watapewa Roho Mtakatifu, baada ya kwenda mbinguni. Katika Yohana 14:25-26 aliwaambia:

> *"Mambo haya nimewaambieni, ningali pamoja nanyi. Lakini Mfariji, ambaye ni Roho Mtakatifu, atakaye tumwa na Baba kwa jina langu, atawafundisha mambo yote, na kuwakumbusha mambo yote, yoyote niliyowaambieni".*

Baada ya Bwana Yesu kuwaacha wanafunzi walihitaji msaada wa kuhubiri na kuweka kanisa la kwanza. Pia Mungu alitumia Roho Mtakatifu (au Mfariji) alikuwepo pale kuwafundisha wao na kuwakumbusha yote ambayo Yesu alisema na kufanya wakati wa maisha yake duniani.

Neno 'Mfariji' maana yake 'aliye itwa kukaribia kusaidia.'

Wakati mwingine Yesu anamtaja Roho Mtakatifu kama vile alikuwa ni mtu. Lakini tayari tumekwisha ona ni wazi kabisa kutoka kwenye Biblia kwamba Roho Mtakatifu ni uwezo wa Mungu.

Kwanini, basi, Yesu sehumu zingine anamsema Roho Mtakatifu kana kwamba alikuwa ni mtu?

Geukia tu katika Zaburi 65, na usome mstari wa 13, ambao unasema:

> *"Malisho yamevikwa na kundi la wanyama; mabonde pia yamefunikwa kwa nafaka; yanashangilia kwa furaha, pia yanaimba".*

Sasa, tunaposoma hivi, inatupa picha ya kuvutia ya nafaka zilizo komaa bondeni; bali hatufikirii kwa maana moja kwamba bonde ni hakika linashangilia na kuimba - hiyo ni njia ya waandishi wa Zaburi katika kuelezea picha.

Hivyo wakati Yesu anamsema Roho Mtakatifu kana kwamba ni alikuwa mtu anafanya hivi au vile, anatuonyesha sisi tu jinsi kitu cha kweli kabisa huyu Roho au uwezo wa Mungu ulivyo.

Mfano mwingine wa aina hii ya lugha ni katika Mithali 3:13-19. Soma mistari hii nawe utaona kwamba mwandishi anazungumzia kuhusu hekima kana kwamba ni alikuwa mwanamke mwema mzuri. Hii ni njia ya maelezo dhahiri yenye nguvu ya kueleza kwamba hekima ya kweli kuhusu Mungu sio tu ni sawa bali pia ni nzuri na timilifu.

Maandiko yanatumia lugha kama hii kwa Roho Mtakatifu au wa Mungu kuonyesha jinsi gani utimilifu wote na nguvu na utendaji wa Mwenyezi Mungu ulivyo. (Utaona mifano mingine ya matumizi ya lugha hii baadaye kwenye kozi).

Roho alikuja kwa wafuasi

Tumekwisha kuona kwamba Yesu aliwaahidi wafuasi wake, Kabla ya kwenda mbinguni. Aliwaambia wakae Yerusalemu, na

> "..... *kusubiri ahadi toka kwa Baba" (Matendo 1:4).*

Aliwaahidi kwamba

> *".....watabatizwa kwa Roho Mtakatifu sio siku nyingi toka sasa" (mstari wa 5).*

Katika Matendo 2 tunasoma jinsi, kama walivyo kuwa wakisubiri pamoja, Roho Mtakatifu alikuja kwa sauti *"kama mvumo wa upepo wenye nguvu",* ukatikisa nyumba walimokuwa ni ishara kwamba wamepewa Roho Mtakatifu. Kutoka wakati huo, waliweza kufanya miujiza, kama Yesu alivyo waahidi.

Yesu alirudi kutoka kuzimu

Yesu baada ya kufufuliwa toka wafu na kupaa kwenda mbinguni, Petro aliwahubiri watu walio kuwa wamekusanyika Yerusalemu kwa ajili ya siku kuu ya Pentekosti. Aliwaambia kwamba Daudi alitabiri kuhusu ufufuo wa Yesu toka wafu. Unabii huu unapatikana katika Zaburi 16, lakini Petro anauzungumza katika Matendo 2:27:

> *"Kwa sababu huta iacha roho yangu kuzimu, wala huta mwacha Mtakatifu wako aone uharibifu."*

Petro anasema kwamba Daudi alikuwa anatabiri kuhusu Yesu Kristo (katika mstari 31):

> *"Yeye (Daudi) akili ona hili kabla alizungumzia ufufuo wa Kristo, kwamba roho yake haikuachwa kuzimu, wala mwili wake haukuharibika."*

Roho ya Kristo (yaani, Kristo mwenyewe) hakuachwa kuzimu (kaburini) kwa sababu Mungu alimfufua siku ya tatu. Mtakatifu wa Mungu hakuona uharibifu.

Katika Ufunuo 1 Yesu ana uzungumzia ufufuo wake mwenyewe, na kisha shadi yake ya kuwa fufua wafuasi wake waaminifu. Anasema:

> *"Mimi ni hai ambaye nalikuwa nimekufa: tazama, mimi nipo hai hata milele, Ameni; na nina funguo za kuzimu na mauti" (Ufunuo 1:18).*

Wafuasi wa Yesu ambao wamekufa wamefungwa kaburini – au kuzimu. Yesu ana funguo. Ana uwezo wa kufungua malango haya atakapo rudi na kufufua wafu kutoka kwenye makaburi yao.

Hades (Kuzimu)

Wakati mwingine “kuzimu” imedhaniwa kuwa ni mahali penye giza ambako roho za walio kufa zinaishi. Tunajuwa kwamba hii haiwezi kuwa sahihi, kwa sababu Biblia inatuambia *“wafu hawajui kitu chochote”* (Mhubiri 9:5). Hawana ufahamu ulipo.

Neno "kuzimu" ni kiswahili ambacho neno hili siku hizi hali tumiki sana, nalo lina maana "penye uficho au palipo funikwa". Hivyo ni neno ambalo limetumika katika Biblia likiwa na maana ya kuwa ni sehemu ya uficho au mahali palipo funikwa pa wafu yaani - kaburi.

KUZIMU maana yake KABURI

Katika Agano la Kale neno kuzimu ni sheol kwa lugha ya Kiebrania. Limetumika katika mafungu haya ya maneno:

Zaburi 49:15
Mwandishi wa Zaburi anasema: “Mungu atantikomboa nafsi kutoka nguvu za **kaburi.**”

Zaburi 55:15
Mwanandishi wa Zaburi anesema: “Mauti na iwashike kwa ghafla na waende chini **kuzimu** haraka.”

Haya maneno mawili ni sawa na neno la asili katika lugha ya Kiebrania (sheol)

Katika Agano Jipya neno kuzimi ni hades.

1 Wakorintho 15:55
Mtume Paulo anasema: U wapi Ewe mauti, uchungu wako? Ku wapi, Ewe **mauti** kushinda kwako?

Ufunuo 1:18
Yesu anasema: “…niliye hai milele na hata milele, Ameni; na nina funguo za **kuzimu** na mauti.”

Haya maneno mawili ni sawa na neno la Kiyunani (hades). Yana maana ya kitu kimoja.

Maneno haya yanaonyesha kwamba katika Agano la Kale na Agano Jipya neno "kuzimu" -lingeweza kutafsiriwa kaburi, kwa hiyo –

KUZIMU maana yake ni KABURI

Kwa sababu hiyo kuzimu sio mahali pa kutisha pa mateso kwa watenda maovu wakifa.

Kwetu Roho amekuja.

Uwezo maalum ulio hitajika kujenga makanisa ya kwanza hauhitajiki tena. (Kuna zaidi kuhusu hili katika somo lijalo). Leo, Mungu ana zungumza nasi kwa Neno Lake.

Tumeona kwamba wale walio andika Biblia walifanya hivyo kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Zaidi ya yote, mara moja Yesu alisema:

"Maneno niwaambiayo, ni Roho na ni uzima" (Yohana 6:63)

Wakati tunasoma Neno la Mungu, tunakuwa katika maana ya kupokea Roho wa Mungu. Huyu anaweza kusababisha mabadiliko ya ajabu katika maisha yetu, akitusaidi kukua zaidi tukimpendeza Mungu. Basi, tusome Neno la Mungu kwa bidii na kwa sala, huku tukikumbuka maneno ya Petro katika waraka wake wa kwanza:

"Kama watoto wachanga, yatamanini maziwa ya kweli ya neno, kwasababu hii muweze kukua" (1 Petro 2:2).

Tumejifunza nini kuhusu Roho Mtakatifu?

[1] Roho Mtakatifu, ni uwenzo wa Mungu.
[2] Biblia iliandikwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.
[3] Yesu alizaliwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.
[4] Manabii wote walikuwa na kipimo cha Roho wa Mungu, bali Yesu alipewa bila kipim.
[5] Uwezo maalum ulio tolewa kwa Roho katika karne ya kwanza ulirudishwa.
[6] Sasa Mungu anazungumza nasi katika Neno Lake, Biblia ambayo imeandikwa kwa Roho Mtakatifu.

Sura za kusoma: Matendo 10:34-43; Yohana 14
Jifunze kwa moyo: Marko 16:15-16

"Naye *aliwaambia, nendeni ulimwenguni pote na muhbiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; bali asie amini atahukumiwa".*

ZAWADI ZA ROHO MTAKATIFU

Soma: Matendo 8

Yesu aliwaahidi wafuasi wake kuwa watapewa Roho Mtakatifu. Aliwaambia:

> *"Ishara hizi zitawafuata wanao amini. Kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watakamata nyoka; na kama wata kunywa sumu, haita wadhuru; na watawawekea mikono wagonjwa nao watapona" (Marko 16; 17,18).*

Wafuasi waliahidiwa kwamba watapewa Roho Mtakatifu na uwezo maalum wa kuwasaidia katika kazi zao. Iliwapasa wasiondoke Yerusalemu, bali wasubiri ahadi kutoka kwa Baba (Matendo 1:4). Hivyo walisubiri kama walivyo ambiwa.

Tayari tumekwisha ona jinsi siku moja (ilikuwa siku ya Pentekosti), wakati walipo kuwa pamoja wote, kitu cha ajabu kilitokea. Nyumba walimo kuwamo ilitikisika, na kulikuwa na sauti *"kama ya mvumo wa upepo wenye nguvu".*

> *"Na wote walijazwa na Roho Mtakatifu, nao wakaanza kunena kwa lugha zingine, kama Roho alivyo wapa usemi" (Matendo 2:4).*

Kwanini zawadi maalum zilizo za roho walipewa wafuasi?

Walihakikisha kwamba ujumbe wa wafuasi ulikuwa kutoka kwa Mungu

Yesu alisulubiwa; Mungu alimfufua kutoka wafu. Alikwenda mbinguni, akawaacha kundi dogo la wafuasi *"Kwenda ... ulimwenguni pote, na kuhubiri injili kwa kila kiumbe" (Marko 16:15).* Ilikuwa ni kazi kubwa. Watu wangewasikiliza? Hakika kamwe wasinge amini habari ya mtu aliye rudi kwenye uhai baada ya kuwa mfu siku tatu. Agano Jipya lilikuwa bado halija andikwa.

***"Wengi** wa hao walio /a/a katika mavumbi ya nchi wata amka, baadhi yao kwenye uzima, na wengine kwenye aibu na kudharauliwa milele" (Danieli 12:2).*

Kwa hiyo kutakuwa na hukumu. Katika 2 Timotheo 4:1 inaonyesha kwamba wale walio hai wakati Yesu akirudi nao pia watahusika kwenye hukumu hii:

> *"(Yesu) atahukumu walio hai na walio kufa atakapo funuliwa na ufalme wake. "*

Wale watakao hukumiwa na kuonekana wanastahili, watapewa nafasi katika Ufalme wa Mungu duniani. Kwa hao, Yesu atasema:

> *"Njoni, ninyi mlio barikiwa na Baba, urithini ufalme ulio tayarishwa kwa ajili yenu toka kuwekwa msingi wa ulimwengu" (Mathayo 25:34).*

Hawa waaminifu watapewa uzima wa milele: uzima ulio kamili na usio na dhambi; wata kuwa sawa na malaika, kama tunavyo soma kwa Luka 20:35,36:

> *'Wale watakao stahili kuhesabiwa kuupata ulimwengu ule, na ufufuo toka wafu, hawaowi wala kuolewa, wala hawafi tena: maana wapo sawa na malaika; nao ni watoto wa Mungu, kwa kuwa ni watoto wa ufufuo."*

> Tumaini la Mkristo ni ufufuo wa mwili na kupewa nafasi katika Ufalme wa Mungu kwenye dunia hii mara Yesu akirudi.

Je, watenda dhambi wanakwenda kuzimu?

Ni kweli kuna sehemu ya kutisha inayo itwa "kuzimu" ambako watu waovu wanakwenda kuteswa mara wakifa? Tumekwisha ona kwamba mtu afapo, uzima wake unakoma kabisa. Hawezi tena kufikiri au kuona chochote. Hivyo wapi, na "kuzimu" ni nini?

Ahadi ya ufufuo na uzima wa milele

Kungekuwa hakuna tumaini kama Mungu asinge mtume Yesu. Mwenyewe Yesu alisems, *"Kama ninyi hamuniamini mimi ndiye niliye, mtakufa katika dhambi zenu"* (Yohana 8:24).

Lakini kwasababu ya kile Yesu alicho fanya katika maisha yake yasio na dhambi na katika kifo chake, tunaweza kuwa na tumaini la uzima baada ya kifo.

> *"Maana Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanae wa pekee, Hi kila amwaminie asipotee, bali awe na uzima wa milele. Kwa maana Mungu hakumtuma Mwanawe ulimwenguni kuuhukumu ulimwengu; bali kwamba ulimwengu kwa yeye uokolewe" (Yohana 3:16,17).*

Dhambi zetu tunaweza kusamehewa kwa Yesu. Yohana Mbatizaji alitoa habari za Yesu kama *"Mwana Kondoo wa Mungu, achukuae dhambi za ulimwengu"* (Yohana 1:29). Ni kwa sababu ya dhambi tunakufa. Basi kama dhambi zetu tukisamehewa kabisa, tukiwa sawa kama Yesu, hatuwezi kukaa tukiwa wafu.

Soma mwenyewe Yohana 6:39,40,44. Utagundua kuwa mara tatu katika mistari hii Yesu anazungumzia kufufuliwa wafu *"siku ya mwisho",* yaani, wakati atakapo kuja duniani tena. Angalia hasa mstari wa 40:

> *"Hay a ndiyo mapenzi yake aliye nituma, kwamba kila mmoja anaye mwangalia Mwana, na kumwamini, apate uzima wa milele: nami nita mfufua siku ya mwisho."*

Yohana 5:28,29 pia inazungumzia ufufuo wa wafu. Yesu alisema:

> *"Msistaajabie hili: kwa maana saa inakuja, ambayo wote walio makaburini watasikia sauti yake, nao watatoka; walio fanya mema, kwa ufufuo wa uzima; na ambao wamefanya mabaya, kwa ufufuo wa hasara kabisa."*

Nabii Danieli analizungumzia jambo hili, tena anaonyesha kuwa baadhi tu ya wale watakao fufuliwa watapewa uzima wa milele:

Hivyo wafuasi walipewa uwezo wa kufanya miujiza na kunena kwa lugha kama ishara kwamba ujumbe wao ulikuwa ni kutoka kwa Mungu. Siku hiyo ya Pentekosti, mara waliondoka na waliwahubiria Wayahudi katika lugha ambazo Mitume hawakuwahi kamwe kujifunza, wala hawakuwahi kuzungumza bali walizungumza kwa uwezo wa Mungu. Sio ajabu habari inawasema watu walio sikia:

> *"Wote walistaajabu na kushangaa, wakisemezana wao wenyewe, Tazama, sio Wagalilaya hawa wanao zungumza? Na jinsi tunawasikia kila mtu kwa lugha yetu tulio zaliwa nayo?" (Matendo 2:7,8).*

Kulikuwa na watu wa mataifa mbalimbali kule Yerusalemu siku ile. Walikuja kwa ajili ya siku kuu ya Pentekosti.

Zawadi za Roho zilisaidia kuongoza kanisa

Kama matokeo ya kuhubiri siku ya Pentekosti, karibu wanaume na wanawake 3,000 walijiunga kwa wafuasi, wakawa Wakristo (Matendo 2-.41).

Na hivyo kanisa la Kikristo lilianza vema.

Lakini fikiria shida zilizo kuwepo. Familia kubwa kama hii ya Wakristo ilihitaji mtu wa kuiongoza na kufundisha, na kuwapa ushauri wa mipangilio ya kufanya ibada. Hawakuweza kujifunza kutoka Agano Jipya, kwasababu lilikuwa bado kuandikwa.

Ndipo zawadi za Roho zilipelekwa, sio kuwathibitishia walio nje ya kweli ya ujumbe wa mitume, bali pia kuwasaidia na kuwafundisha Wakristo wa kwanza, na kuweka makanisa ya kwanza katika utaratibu.

Hizi zawadi zilikuwa ni nini?

Tayari tumekwisha ona kwamba mitume waliweza kunena kwa lugha ambazo hawakuwahi kamwe kujifunza. Pia waliweza kuponya wagonjwa. Katika 1 Wakorintho 12:4-22 mtume Paulo anaonyesha jinsi washirika mbalimbali wa kanisa walipata vipawa tofauti-tofauti, na namna kila mshirika alifanya kazi kwa ajili ya mema kwa wengine. Kisha mistari 28-29

anatowa orodha ya zawadi:

> *"Na Mungu wengine amewaweka katika kanisa, kwanza mitume, pili manabii, tatu waalimu, baada ya hapo miujiza, kisha zawadi za uponyaji, misaada, uongozi na lugha mbalimbali."*

Zawadi za Mungu haziwezi kununuliwa

Wafuasi mara walipo pokea zawadi ya Roho Mtakatifu, walianza kazi ya kuhubiri. Mfuasi wa Yesu aliyeitwa Philipo alishuka kwenda pande za Samaria naye alianza kufundisha watu kule. Wengi walio msikiliza maneno yake na kuamini kuhusu Yesu na Ufalme wa Mungu unao kuja, walibatizwa.

Miongoni mwao walio batizwa kulikuwa na mtu aliyeitwa "Simoni Mchawi". Alikuwa mfanya-ajabu ambaye aliwadanganya watu wa Samaria kwa muda mrefu kwa mbinu zake za ujanja.

Wakati mitume waliposikia kule Yerusalemu kuwa kule Samaria kuna waongofu wapya, waliwatuma Petro na Yohana kusaidi katika kazi.

Sasa Petro na Yohana, wakiwa ni mitume, waliweza kutoa uwezo wa Roho Mtakatifu kwa wengine kwa kuwawekea mikono. (Hii ilikuwa ni kitu fulani tu mitume wa kwanza waliweza kufanya.) Simoni, akisimama karibu, alipo ona watu hawa wawili wanaweka mikono juu ya wanafunzi wapya na kupitisha kwao Roho Mtakatifu alistaajabu. Pengine alifikiri yeye mwenyewe: "Utajiri gani na uwezo **nita** kuwa nao, iwapo **niki** weza kutoa hizi zawadi."

Hivyo kweli alitoa fedha ili anunue zawadi toka kwa Petro.

Hiki kilikuwa ni kitu cha kutisha kufanya! Sio ajabu Petro alimwambia:

> *"Huna sehemu wala bahati katika jambo hili: kwa maana moyo wako haupo sawa machoni pa Mungu. Kwa hivyo tubu uovu wako, na umuombe Mungu, kama labda mawazo yako ya moyo yaweze kusamehewa. Kwani ninaona una uchungu na kifungo cha uovu" (Matendo 8:21-23).*

MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIAN NA 23

DHAMBI NA MATOKEO YAKE (Sehemu 2)

Soma: Mhubiri 3 **Nini - baada ya kifo?**

Kuna mawazo mengi tofauti kuhusu kile kinacho tokea wakati tukifa. Watu wachache wanapenda kufikiri kwamba wakati wakifa, huo utakuwa ni mwisho wao. Hapa pana baadhi ya mawazo waliyo nayo watu:

- wengine wanadhani wataonekana tena wakiwa kama wanyama (hii imeitwa kuvaa kiwiliwili);
- wengine wanafikiri kuna kitu fulani ndani yao ambacho kinakuwa hai mahali fulani
- wengine wana amini hakuna tumaini kabisa la aina yoyote la uzima baada ya kufa,
- kuna watu wana amini kutakuwa na siku ya ufufuo wa wafu, itafuatia hukumu, na uzima wa milele kwa waaminifu.

Biblia inasemaje?

Tayari kamatulivyo ona, kifo ni adhabu kwa ajili ya dhambi. Mauti ni kutokuwa na uhai hali isiyo na mawazo yoyote au ufahamu wowote kabisa. Kifo ni mwisho wa uzima na hakuna kiungo ndani yetu kinacho kuwa hai.

> *"Walio hai wanajuwa watakufa; bali wafu hawajui kitu chochote, wala hawana ijara tena; maana kumbukumbu lao limesahauliwa. Pia, mapenzi yao na machukio, na husuda yao imeporea sasa: wala hawana sehemu yoyote zaidi tena katika jambo lolote linalofanyika chini ya jua." (Mhubiri 9:5,6)*

Je, kwetu sisi ina maana hakuna tumaini? Kuna tumaini ng'ambo ya kaburi?

Mfalme Hezekia alipo ambiwa kwamba atakufa alihuzunika. Alitaka kukaa akiwa mzima kwa sababu alijua hakuna chochote mautini. Alisema:

> *"Kwa kuwa kaburini hakuwezi kukusifu, kifo hakiwezi kukuadhimisha; wale washukao shimoni hawawezi kuitarajia kweli yako" (Isaya 36:18).*

Badala yake aliseme, *"Aliye hai, aliye hai atakusifu"* (Isaya 38:19). Kama alikuwa amekufa asingeweza kumsifu Mungu.

Ni vipi kuhusu Mfalme Daudi? Tuna ambiwa kwamba hakwenda mbinguni (Matendo 2:34) -ingawa ameitwa mtu wa moyoni mwake Mungu.

Watu wote wamehukumiwa kifo kwa sababu ya dhambi. Hawaendelei kuishi kwa namna ingine baada ya kufa.

Lakini Biblia inatuambia hatuna tumaini la uzima pasipo Kristo.

Muhutasari

1. Mungu ali muumba Adamu toka mavumbi ya ardhi.
2. Alimfanya aishi, kwa kumpulizia puani mwake pumzi ya uhai.
3. Mungu alimpa amri Adamu. Alimwambia kwamba iwapo akivunja amri hii, adhabu itakuwa kifo.
4. Adamu na Eva walivunja amri yake. Wakawa viumbe wanao kufa.
5. Watu wote wamezaliwa kutoka kwa Adamu, na wamerithi mwili wenye dhambi. Watu wote wantenda dhambi na kufa.
6. Neno "nafsi" maana yake uzima au uwepo, na mara kwa mara linataja mtu.
7. Fungu la maneno *"roho isiyo kufa"* halipatikani katika Biblia.
8. Kifo ni adhabu ya kufanya dhambi.
9. Mauti ni hali ya kukosa ufahamu. Hatuna sehemu ndani yetu ambayo inaendelea kuwa hai tunapo kufa.

Sura ya kusoma: Mhubiri 9
Mstari wa kujifunza: Zaburi 146:4

"Pumzi yake hutoka, yeye anarudi mavumbini; katika siku hiyo mawaza yake yapotea."

Wakati huo Simoni aliogopa, na alimwomba Petro amuombee. Hatuja ambiwa baada ya hili palitokea nini.

Habari inatonyesha wafuasi wa kwanza walitumia uwezo wa Roho Mtakatifu wakati walipo wahubiria watu kuhusu Yesu na Ufalme.

Soma Matendo 8:15-25 na ufahamu maana zifuatazo:

1. Mstari wa 18 unasema kwamba katika kuwawekea mikono ya **Mitume** ndipo walipewa Roho Mtakatifu.
2. Simoni hakupata zawadi za Roho Mtakatifu wakati alipo batizwa.
3. Mitume Petro na Yohana waliwapa waamini wapya walio batizwa zawadi za Roho Mtakatifu baada ya kuwaombea na kuweka mikono juu yao (hii ilikuwa ni njia ya baraka au kubarikiwa).
4. Hata baada ya Simoni kupata Roho Mtakatifu katika njia hii hakuweza kutoa kwa wengine. Jinsi ilivyo alitaka vibaya mno.

Hii inaonyesha kwamba ilikuwa ni **Mitume** tu walio toa zawadi za Roho Mtakatifu Wakati walipokufa zawadi hazikuweza kutolewa na zilitoweka na kizazi cha watu wale.

Mwisho wa zawadi

Tayari tumekwisha ona kwamba katika siku za Wakristo wa kwanza, kulikuwa hakuna Agano Jipya - lilikuwa halija andikwa; na tumedokeza kwamba hii ni sababu moja kwanini zawadi hizi zilikuwa za lazima.

Leo, tunaweza kusoma maisha ya Bwana Yesu, na tunaweza kusoma nyaraka ambazo mitume waliwaandikia makanisa ya siku zao. Lakini **walikuwa** hawana habari iliyo kuwa imekwisha andikwa, hivyo basi, mitume, manabii na waalimu pamoja na uwezo maalum kutoka kwa Mungu ulikuwa ni wa lazima sana kusaidia kanisa la kwanza.

Wakati maandiko ya Agano Jipya yalipokamilika, kulikuwa hakuna tena hitaji la uwezo huu maalum toka kwa Mungu. Yote ambayo Wakristo wanahitaji kujua yameandikwa kwa ajili yao ndani ya Biblia. Hivyo karama za Roho ziliondolewa.

Mtume Paulo alisema hili lingetokea. Katika 1 Wakorintho 13:8 twasoma:

"Upendo haupungui: bali ukiwapo unabii (yaani, karama ya kutoa unabii), atadimika (au utakoma); zikiwapo lugha (yaani, karama za kunena kwa lugha), zitakoma; yakiwapo maarifa (karama ya elimu) itatoweka. "

Ilionekana kwamba karama hazikuondolewa mara moja, kwa wakati halisi wakati Agano Jipya lilipokamilika: bali ni kwamba kadri wakati ulivyokwenda, wale walio kuwa na zawadi hizi walikufa, na hawakutoa kwa Wakristo walio wafuata.

Je, kuna yeyote aliye nazo hizi zawadi leo?

Watu wengine wanadai wanazo karama za roho. Zaidi wanadai wanaweza kunena kwa lugha na kuponya wagonjwa. Tutawezaje kuwajaribu wale wanao dai wanafanya miujiza kwa Roho wa Mungu?

1. Tunajikumbusha wenyewe kwamba mtume Paulo alisema kwa 1 Wakorintho 13, kuwa wakati utakuja wa zawadi za roho zitakoma. Muda huo ulikuja lini, kama sio mapema baada ya Agano Jipya lilipokamilika? Haiwezi kuwa na ujaji wa Ufalme, kwasababu kutakuwa na zawadi zaidi ya wakati ule zilipokuwepo. (Zawadi za Roho Mtakatifu, kwa kweli, zimeitwa *"nguvu za zamani zijazo, ulimwengu ujao"* (Waebrania 6:5), na wanafunzi wa kwanza walikuwa na "malimbuko" ya karama hizi ambazo zitatolewa bure katika Ufalme.)
2. Tunafahamu kwamba karama za Roho Mtakatifu zilitolewa ili kusaidia kanisa la kweli. Kanisa la kweli linaamini na kuhubiri Neno la Mungu. Wengi wao wanao dai kuwa na nguvu hizi leo - kama sio wote - wanahubiri mambo ambayo hayakufundishwa katika Neno la Mungu. Inatupasa, kwa hivyo, tukatae madai yao.
3. Inatubidi tukiri kwamba hatu ingizi moyoni inayo itwa mingi miujiza. Tiba nyingi mapema zinaonekana kuwa sio tiba; mingine inaweza kuelezwa kisayansi. Watu wenye uwezo wa kuwatia watu hali ya usingizi na kumfanya atende mambo yalio amriwa katika usingizi huo mara nyingi yanaweza kuleta matokeo hayo. Hakuna hata mmoja wao anayeweza kufufua wafu.

Pana mifano mingi zaidi tunaweza kutoa ili kuonyesha kwamba neno nafsi (roho) maana yake mtu au kiumbe. (Ukweli neno lililo tafsiriwa "nafsi" pia limetumika kwa wanyama; angalia katika Mwanzo 1:21,24; 2:19; 9:10. Katika mambo haya limetafsiriwa "kiumbe")

Yote haya yanathibitisha kile anachosema Mhubiri 3:19-20:

"Kwa maana linalo watukia wanadamu linawatukia wanyama; kitu kimoja kinawatukia wote: kama anavyo kufa huyu, ndivyo anavyokufa mwingine; naam, wote wanapumzi moja; kwa hiyo mwanadamu hana chakumpita mnyama: maana yote ni ubatili. Wote huenda sehemu moja; wote wanatoka mavumbini, na mavumbini wanarudi tena."

Hakuna tofauti katika mauti kati ya mwanadamu na mnyama. Mnyama hana sehemu ambayo huenda mbinguni anapokufa yoyote zaidi ya mwanadamu. Wote wawili wana miili isio na uhai wanapo acha kupumua.

"NAFSI" maana yake UZIMA, MFU, KIUMBE au UWEPO

Tazama mafungu haya ya maneno ambayo yanatuonyesha sisi kile kinacho tokea wakati tukifa. (Endelea na ndipo uweza kusoma yote.)

Zaburi 146:4	"Pumzi ya mwanadamu hutoka, anarudi mavumbini, katika siku hiyo hiyo mawazo yake yapotea."
Mhubiri 9:5	"… wafu hawajui kitu chochote ...
Zaburi 6:5	"Mautini hakuna kumbukumbu lako; kaburini ninani atakushukuru wewe?"
Zaburi 39:13	"Niachilie, ile niweza kupata nguvu, kabla sijaondoka, nisiwepo tena."
Zaburi 115:17	"Wafu hawamsifu BWANA, wala waendao chini kwenye ukimya."

Mafungu yote haya yanaonyesha kwamba wafu haawezi kufikiri.

"Kwasababu hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na mauti kwasababu ya dhambi; na hivyo mauti yamewafikia watu wote, maana wote wamefanya dhambi"

(Warumi 5:12).

(Hii haina maana kwamba watu wote ni wauaji au wazinzi au waongo. Yasio mema na mawazo machafu, kiburi, ubinafsi, hasira mbaya - udhaifu huu wote wa kila siku ni sawa kama dhambi mno mbele za Mungu.)

Hakuna hata mmoja wetu atakwenda mbinguni wakati tukifa. **Hakuna kitu kama hiki "roho isio kufa".** Biblia haitaji roho ambazo hazifi. Hakuna chochote kinacho endelea kuwa hai mtu akifa. Hakuna 'kisicho kufa' au chembe ya "Mungu" ndani ya mwanadamu.

Nafsi (roho) maana yake ni uhai, mtu, kiumbe hai

Chini ni orodha ya baadhi ya sura za maneno katika Biblia ambapo neno hili "nafsi" LIMETUMIKA. (Sura za maneno zimetolewa kutoka A.V. au KJV. Katika Biblia yako ya Union Version katika Kiswahili, tafsiri inaweza kutofautiana na A.V. au KJV lakini maana bado itakuwa ni ileile.) Tazama mwenyewe na uone kama unakubaliana na fafanuzi.

ILIPO TAJWA	UFAFANUZI
Mwanzo 46:15	Watoto walio hai wa Yakobo wanaitwa "nafsi" katika mstari huu.
Mwanzo 46:26	"Nafsi zote" maana ya wazi wazi ni "watu wote".
Mambo ya Walawi 5:2,17	Nafsi zinaweza kufanya dhambi (kwa maneno mengine **watu** wanaweza kufanya dhambi).
Mambo ya Walawi 17:12	Hakuna nafsi ilio kula damu – hakuna mtu alikula damu.
Yoshua 10:28,30,32,35,37	Nafsi zote (watu) ziliharibiwa kabisa. (Elewa “nafsi” zinaweza kuharibiwa!)
Yoshua 11:11	Waliziua nafsi zote kwa hiyo hakuna hata mmoja aliye baki anapumua.
Ezekieli 18:4,20	“Roho itendayo dhambi, itakufa.” Sasa Nafsi hufa! (Hii ina maana kwamba kama tukitenda dhambi tu tunakufa.)
Matendo 27:37	Kulikuwa na nafsi 276 ndani ya merikebu. Nafsi hapa dhahiri maana yake “watu”.

Mungu anaweza, na hata sasa anafanya, kazi katika Roho Wake leo, lakini **haruhusu watu kutumia Roho Wake.** Wale ambao wana amini yote yalio andikwa katika Biblia hawata dai kuwa wana zawadi za Roho. Wanajua kwamba zawadi zilikuwa ziondoshwe mapema baada ya maandiko ya Agano Jipya yalipo kuwa yamekamilika.

Hata sasa Mungu ana tenda kazi

Hatuna tena uwezo wa kufanya miujiza na kunena kwa lugha. Roho Mtakatifu wa Mungu bado yupo kazini leo kama, kwa mfano, wakati Mungu anajibu maombi; na hata sasa Mungu pia anasema katika Neno lake. Wakati tunasoma Biblia, tunakuwa katika maana ya kweli, tunafundishwa na Roho wa Mungu. Kama tunataka kumpendeza Mungu, wakati huu, hebu tuonyeshe kwamba yote aliyo kwisha fanya kwa ajili yetu tushukuru kwa kusoma Neno lake, na kujifunza yote tuwezayo toka ndani yake.

Kwa ufupi

1. Karama za Roho Mtakatifu zilitolewa kwa Wakristo wa kwanza.
2. Zilikuwa kwa ajili ya makusudi matatu:
   (a) Kukamilisha Agano Jipya
   (b) Kuwa ishara kwa wasio amini;
   (c) Kusaidia kujenga kanisa la kwanza.
3. Zilitolewa tu **hata** Agano Jipya lilipokwisha andikwa; baada ya hivi zilitoweka.
4. Tangu wakati ule hakuna mtu aliye weza kufanya miujiza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.
5. Watu wale wanaodai wanafanya miujiza leo wanaweza kuwa na uwezo mgeni, kama tulivyo taja hapo juu. Lakini **sio** nguvu za Roho Mtakatifu.

Sura za kusoma: 1 Wakorintho 13 na 14
Jifunze kwa moyo: 1 Wakorintho 13:8

"Upendo haupungui neno: bali ukiwapo unabii utaadimika; ukiwapo kunena kwa lugha kutakoma; yakiwapo maarifa yatatoweka. "

MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIANO NA 22.

DHAMBI NA MATOKEO YAKE (SEHEMU 1)

Soma: Mwanzo 2 na 3

Ulimwengu umo katika vurugu! Vita, Njaa, Magonjwa, Vifo, Matendo ya kuvunja sheria, Utumiaji nguvu ... Mungu aliuumba ulimwengu mzuri. Mwanadamu ameuharibu. Tabia ya dhambi ya mwanadamu na uchoyo wake, ubinafsi, wivu na uasi vimeharibu jamii na dunia hii.

Ni wapi yote yalianza kwenda vibaya?

Hapo mwanzo Mungu alimuumba mtu wa kwanza, Adamu. Aliumbwa kutokana na mavumbi ya ardhi, na tunasoma kuwa:

> *"Bwana Mungu alifanya mtu wa mavumbi ya ardhi, na alimpulizia puani mwake pumzi ya uhai; naye mtu akawa nafsi hai" (Mwanzo 2:7).*

Mungu alimtayarishia Adamu bustani nzuri ya kuishi na kisha alimpa na mke wake, Eva. Kwenye hatua hii, Adamu na Eva hawakuonyeshwa kama wangemtii Mungu au la. Hawakujaribiwa bado. Mungu aliwapa agizo rahisi:

> *"Kila mti wa bustani upo huru kula; bali mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile: kwa maana siku utakapo kula hakika utakufa" (Mwanzo 2:16-17).*

Adamu na Eva walikuwa na tendo la kuchagua

Ama wangaweza kumtii Mungu au wangeweza kumuasi na kula matunda ya mti uliokatazwa. Walikuwa na hiari. Mungu hakuumba watu wasio na uchaguzi kama kwamba watatii au la. Mungu aliwataka wanaume na wanawake ambao wangechagua njia zake kwasababu ya kumpenda na kumheshimu. Nyoka alikuja kwa mbele na akawadanganya Adamu na Eva. Nyoka alisema hawata kufa ikiwa watakula matunda yalio katazwa,

na kwamba badala yake watakuwa kama miungu, kujua mema na mabaya. Adamu na Eva walitaka zaidi kuwa kama malaika. Walichagua kula matunda. Walitenda dhambi na walimuasi Mungu.

Adhabu

Mungu alisema watakufa ikiwa watamuasi. Hivyo Adamu na Eva walihukumiwa kifo na walifukuzwa kutoka kwenye Bustani ya Edeni.

Ingawa waliishi muda mrefu baada ya hili, wakawa viumbe wanao kufa - na sawasawa kama wewe na mimi, wakawa wanachoka na kuugua, kuzeeka, na mwishowe kufa.

Kifo ni nini?

Kifo kilikuwa ni adhabu kwa ajili ya dhambi. Mungu alisema:

> *"Wewe ni mavumbi, na mavumbini utarudi" (Mwanzo 3:19).*

Kwa sababu hiyo mwili wa Adamu ulioza wakati alipokufa na kurudi mavumbini alikotwaliwa. Kumbuka, Mungu alimuumba Adamu kutoka mavumbi ya ardhi na kisha Mungu alimpulizia pumzi ya uhai ndani yake kabla hajawa "nafsi hai".

MAVUMBI ongeza PUMZI = NAFSI HAI

Basi wakati Adamu alipokufa,

NAFSI HAI toa PUMZI = NAFSI MFU
hiyo ni, NAFSI HAI pasipo PUMZI ikawa MAVUMBI

Sehemu ya Adamu haikuendelea kuishi mbinguni. Bila shaka hakuna! Kifo chake kilikuwa ni adhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi, na mauti maana yake ni mwisho wa mafuatano yote ya mambo katika maisha.

Kifo cha Adamu hakikuwa na tofauti na kifo kinachotupata sisi. Sote tunafanya dhambi na kwasababu hiyo sote tunakufa.

Kama unataka kujifunza zaidi njia ya Mkristo wa kweli anavyopaswa kuishi, basi ni lazima ujifunze Biblia. Ili kukusaidia; Kanise la Christadelphian Bible Mission limechapisha kijitabu kuhusu mafunzo ya Biblia kaitka somo hili muhimu.

Lina itwa Kuishi katika Ukweli. Unaweza kupata nakala kutoka Kanisa la Christadelphian, au kutoka anuani iliyoandikwa katika kijitabu hiki.

CBM Publishing
32 Blenheim Road, Far Cotton
Northampton, England. NN4 7SG

ISBN 1 902059 08 -5
Registered Charity Number: 248979 / 1020558
Company Number: 2796412

MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIAN 20-23
Correspondence Course Lessons 20-23